***OFISI YA RAIS – TAMISEMI***

***HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI***

Shule ya Sekondari Lyamungo,
S.L.P. 3020,
**MOSHI.**

Tarehe ……………………….

SIMU
Mkuu wa Shule: 0787173611/0716018848
Makamu Mkuu wa Shule 1: 0658208461
Makamu Mkuu wa Shule 2: 0713990090

Kumb. Na. UT/LY/43B/112

MZAZI/MLEZI/ MFADHILI WA MWANAFUNZI:
………………………………………………………………………………………………

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LYAMUNGO MWAKA 2022/2023</u>**

**1. UTANGULIZI:**

Kwa niaba ya Jumuiya ya Shule ya Sekondari Lyamungo ninayo furaha kukujulisha kwamba Mwanao ……………………………………………………………………………………………amechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari Lyamungo kidato cha tano (5) kwa mwaka huu 2022/2023 katika tahasusi ya ……………………………

Shule ya Sekondari Lyamungo iko umbali wa Km. 24 Kaskazini Magharibi ya Mji wa Moshi katika Wilaya ya Hai Mkoa wa Kilimanjaro. Shule iko katika mazingira mazuri ya mwanafunzi kusoma na kuweza kufaulu vizuri kama atatia bidii katika masomo yake. Mwanao aitumie nafasi hii vizuri aliyopewa na serikali akizingatia kwamba wenzake wengi wamebaki nyumbani kwa kukosa nafasi hii.

Aidha nampongeza tena mwanao kwa kuchaguliwa kwake na kujiunga na shule yetu. Mwanao anatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe ………………….. bila kuchelewa tayari kwa kuanza masomo tarehe ……………………..

Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe ……………………………. ili kutoa nafasi ya kurudisha majina ya wanafunzi wasiofika shuleni Wizarani ili wanafunzi waliokosa nafasi waweze kupangwa kujazia nafasi hizo.

**2. USAFIRI WA KUJA SHULENI:**

Ufikapo Moshi Mjini standi kuu uliza na upande magari yaendayo Kibosho Umbwe kupitia barabara ya Arusha (Kibosho Road). Mwisho wa magari hayo yanapogeuzia ndipo hapo utakapoteremkia panaitwa Lyamungo Kijiweni.

Ukishuka hapo Kijiweni, uliza shule ya sekondari ya Lyamungo ilipo utaelekezwa kutoka hapo Kijiweni utatembea umbali wa mita 300 hadi kufika shuleni au usafiri wa pikipiki ni shilingi elfu moja tu (1,000/=). Ukifika shuleni utaripoti na kupokelewa na Makamu Mkuu wa Shule au Mwalimu wa usajili wa wanafunzi, wote watakuwepo ofisini kwa huduma za mapokezi.

**3. <u>MAHITAJI YA KULETA SHULENI MWANAFUNZI:</u>**

**(a) Sare ya Shule**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa kuzingatia maadili ya uanafunzi kama ifuatavyo;

- Mashati meupe mawili (2) mikono mirefu – (Tomato)
- Tai ndefu rangi ya kijivu (light ash gray).
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi (2) vya kamba na visivyo na urembo wowote.
- Soksi ndefu za rangi nyeusi jozi 2 au zaidi.
- Vifaa vya michezo ni kama ifuatavyo:
    - CBA, PCB na CBG – jezi ya rangi ya bluu (light blue)
    - EGM, HGE, HGL, HGK na HKL – jezi ya njano.
    - Raba rangi yoyote
- Track suit ya rangi ya kijivu (light ash gray).
- Masweta mawili ya rangi ya kijivu ( light ash gray).
- Suruali mbili za rangi ya kijivu (light ash gray) ziwe na marinda mawili na chini isipungue nchi 15 (Mzunguko wa chini uwe na Turn up).
- Buti za mvua (rain boots) - zitavaliwa kipindi cha mvua na shambani.

**MUHIMU: Marinda mawili kwenye suruali ni lazima**.

**(b) Nguo za kushindia**.

Kila mwanafunzi aje na suruali mbili nyeusi, ''T-shirt'' mbili za rangi ya kijivu zenye kola (maarufu kama "Form six").

**ZINGATIO: Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo nyingine hivyo asije na nguo tofauti na maelekezo**.

**(c) Ada na michango wanafunzi wanayotakiwa kuleta shuleni:**

Mwanafunzi anatakiwa alete ada na michango mingine kama ifuatavyo:-

- Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh. 70,000/= au Tshs. 35,000/= kwa Muhula mmoja
- Shilingi 8,000/= za kitambulisho na nembo ya shule.
- Shillingi 15,000/= za uchakavu /ukarabati wa samani.
- Shilingi 20,000/= Taaluma.
- Shilingi 30,000/= Ulinzi, Upishi na vibarua wengine.
- Shilingi 20,000/= Mitihani.
- Shilingi 5,000/= Tahadhari. **Hairudishwi.**
- Matibabu 10,000/=

- Karatasi **A4** Ream **1 (karatasi za kutolea kopi)**

Michango yote ya shule itawekwa kwenye Akaunti za shule kama inavyoonesha hapa chini:-

| JINA LA A/C | AINA YA MCHANGO | JUMLA |
|---|---|---|
| LYAMUNGO CAPITATION AKAUNTI NAMBA **40101200109** | ADA | 70,000/= kwa mwaka (35,000/= Kwa muhula). |
| LYAMUNGO DEVELOPMENT AKAUNTI NAMBA **40101200110** | Ukarabati wa samani | 15,000/= kwa mwaka |
| LYAMUNGO GENERAL AKAUNTI NAMBA **40301200125** | (a) Michango mingine yote inayobaki | 93,000/= Mara moja kwa mwaka. |

MUHIMU*: **Akaunti zote ziko benki ya NMB***

Baada ya kufanya malipo hayo kupitia Benki , mwanafunzi atatakiwa kuleta Shuleni HATI YA MALIPO (**Bank Pay in Slip)** ili aweze kukatiwa stakabadhi ya Serikali kwa malipo hayo aliyoyafanya. Tafadhali mwanafunzi asilete fedha taslimu shuleni kwani atalazimika kurudi kuziweka Benk (epuka usumbufu), unaweza kuweka katika Tawi lolote la **NMB** Nchini sio lazima **Moshi.**

**MUHIMU: Hakikisha fedha unaziweka benki Mzazi /Mlezi mwenyewe na mtoto apewe "PAY IN SLIP."**

**ZINGATIA:**

Tafadhali weka ada kwenye akaunti ya ada, vivyo hivyo Michango ya shule kwenye akaunti ya michango ya shule, usichanganye ukaweka ada kwenye akaunti ya michango au ukaweka michango kwenye akaunti ya ada kwani itakugharimu kulipa mara mbili; shule haitahusika katika hilo endapo utaenda kinyume.

**(d) Vifaa vya usafi shuleni:-**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kufanyia usafi awapo shuleni, na viwasilishwe ofisi ya Msajili wa wanafunzi wakati wa kuripoti.

- PCB - dawa ya kusafishia choo lita 5, soft broom na reki.
- CBA - dawa ya kusafishia choo lita 5 na jembe lenye mpini.
- CBG - mopper complete, soft broom na water squeezer.
- EGM - dawa ya kusafishia choo lita 5 na jembe lenye mpini.
- HGE – brashi za kusugulia choo 2, chelewa, brashi ya kufutia buibui na panga (lililonolewa).
- HGL – mopper 2 na ndoo yake 1, soft broom na ufagio wa chelewa.
- HGK – mopper 2 na ndoo yake 1, soft broom na ufagio wa chelewa.
- HKL – mopper 2 na ndoo yake 1, soft broom na ufagio wa chelewa.

***MUHIMU: Vifaa vyote hivi vinapatikana Moshi mjini na kijiweni.***

**(e) Mahitaji ya Bweni**

Kila mwanafunzi atahitajika kuwa na vifaa vifuatavyo bwenini.

- Godoro moja la sponge size 2 ½ x 6
- Shuka rangi ya Pink pea 2
- Mto na foronya yake rangi ya Pink 1
- Taulo moja

- Blanket 1 kuna baridi kali.
- Sweta jeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa prepo na lisiwe na kofia.
- Kanda mbili za kuogea
- Sanduku la chuma lenye kufuli imara.
- Chandarua ya pembe nne rangi nyeupe
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko vya aluminiamu.
- Ndoo **1** ya plastiki lita **10** kwa matumizi binafsi.

**(f) Mahitaji ya Darasani:-**

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na mahitaji ya darasani kama ifuatavyo:-

- Madaftari makubwa ya kutosha, kalamu, rula na penseli – vifaa hivi vinapatikana duka la shule.
- "Mathematical set" 1 na "Calculator" kwa wanafunzi wa **CBG, HGE, CBA, EGM na PCB**.
- Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi.

**(g) Fomu mbalimbali za mzazi/ mwanafunzi za kuja nazo:-**

Baada ya Mwanafunzi/ Mzazi kukiri kwa kusaini fomu hizo, zitaletwa shuleni ili iwe rahisi kwa mwanafunzi kurudishwa nyumbani kama ataenda kinyume na taratibu za shule

a) Fomu ya Mwanafunzi kukiri kukubali kufuata sheria za shule bila shuruti.
b) Fomu ya Mganga wa Mkoa/ Wilaya (Appendex "B")
c) Fomu ya Mzazi/ Mlezi.
d) Fomu ya maelezo binafsi yahusuyo Mwanafunzi.
e) Sheria na kanuni muhimu za shule. Isainiwe na Mzazi pia.

**(h) Huduma zitolewazo na shule**

Shule ya Sekondari Lyamungo inayo miradi mingi ambayo hutoa huduma shuleni. Baadhi ya miradi hiyo ni:-

- Duka la shule
- Kantini.
- Saloon.

Mwanafunzi anashauriwa kutobeba mizigo na vitu vingi vya kuja navyo shuleni kama Madaftari, sabuni, kalamu, vyombo vya kulia chakula, dawa ya meno kwani vyote vinapatikana katika duka la shule.

**ZINGATIO:**

i) Shule haitoi chakula maalumu kwa wanafunzi wagonjwa (**Special Diet**). Shule inatoa chakula kulingana na ratiba ya chakula kwa wanafunzi wote. Mzazi anashauriwa kumpatia mtoto wake fedha kama atahitaji chakula maalumu ili mtoto ajigharamie kupata chakula kwenye kantini ya shule. Vile vile shule haitoi fedha kwa ajili ya matibabu ya mwanafunzi. Mzazi anashauriwa kumpatia mwanae fedha kiasi za tahadhari kwa ajili ya matibabu binafsi. Fedha hizo atakaa nazo mwanafunzi mwenyewe ama akipenda atatunziwa na shule.

**MUHIMU:**

Ninasisitiza kwamba hakuna mwanafunzi atakayepokelewa bila kukamilisha mahitaji hayo yaliyotajwa. Mzazi anashauriwa kumwandaa mwanae kikamilifu ili mwanafunzi huyo asirudishwe nyumbani. Aidha mwanafunzi **haruhusiwi** kuleta shuleni **REDIO, SIMU, HEATER AU PASI** kwani vitu hivyo ni **marufuku** shuleni. Mzazi anashauriwa kufanya mawasiliano na mtoto wake pale inapolazimu

kupitia simu ya mkuu wa shule tu **0787173611/0716018848**. Pia mwanao aje na “**RESULTS SLIP**” yake ni muhimu sana.

Kwa sababu shule ina uhaba wa vitabu mzazi anashauriwa kumnunulia mwanaye vitabu vinavyoendana na masomo yake, wanafunzi wanavifahamu vitabu hivyo.

**Mwisho:** Namtakia mwanao maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa Lyamungo shule ya Sekondari

***KARIBU! SANA NA HONGERA KWA KUCHAGULIWA!***

***NB: ZINGATIA***

- **Simu/ Redio/ Heater na Pasi haviruhusiwi kabisa shuleni.**
- **Kila mmoja aje na “Result Slip” yake.**
- **Mji wa Moshi ni msafi sana hivyo hakikisha hutupi uchafu wowote chini au kutema mate, faini ya makosa hayo ni Tsh. 50,000/=**
- **Siku ya kufungua shule wanafunzi wafike kabla ya saa 12:00 jioni na siku zingine za kazi wafike kabla ya saa 9:30 alasiri.**

**ASANTE,**

**………………………………………….**

**YONAFIKA E. GODSON**

**MKUU WA SHULE**

## KIAMBATANISHO A

## SHERIA ZA SHULE

Sheria zote zimewekwa kwa wanafunzi ili kuwawezesha kufikia lengo lao la kuwa shuleni hivyo muda wote lazima mwanafunzi azingatie sheria zifuatazo;

1. Kuwa mwanafunzi unapaswa kutambua kuwa wakati wote unaishi ndani ya utaratibu wa kiuanafunzi ndani na nje ya shule.
2. Kuongeza muda wa ruhusa halali mfano kwenda hospitali, mjini n.k. ni kosa linasababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kuchelewa kurudi shuleni wakati wa likizo.
4. Kutii viongozi ni wajibu wa kila mwanafunzi. Wanafunzi wawaheshimu na kuwatii waalimu, wafanyakazi wasio waalimu, wageni wote wanaoitembelea shule, viongozi wote wa taifa na viongozi wa wanafunzi.
5. Wageni hawaruhusiwi kufika au kuingia bwenini.
6. Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya eneo analotakiwa kuwepo.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kuendesha au kushiriki katika vyama ambavyo havitambuliwi na uongozi wa shule au kuchezea vilabu vya michezo nje ya shule.
8. Nywele fupi zisizozidi urefi wa robo inchi na daima ziwe zimechanwa. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara, panki/kisahani au kiduku.
9. Ruhusa ya kutoka mje ya shule hutolewa na mkuu wa shule au mwalimu mwingine kwa idhini ya mkuu wa shule. Kibali cha kushiriki mazishi hutolewa kwa mwanafunzi aliyefiwa na baba, mama, au ndugu wa kuzaliwa tu.
10. Wakati mwanafunzi anapokuwa nje ya shule kwa ruhusa ni lazima awe amevaa sare ya shule, pia anapokwenda likizo au wakati wa kurudi.
11. Haruhusiwi mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani mbali na nguo alizoagizwa na shule.
12. Hairuhusiwi mwanafunzi kuhama chumba au bweni bila kibali vinginevyo ataadhibiwa.

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki, kukutwa na au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

# KIAMBATANISHO B

# SHULE YA SEKONDARI LYAMUNGO

# S. L. P 3020.

# MOSHI.

**FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI KUFUATA SHERIA ZA SHULE BILA SHURUTI**

Mimi………………………………………………………….. (Jina la Mwanafunzi)

*NINAKUBALI/SIKUBALI kufuata sheria zote za shule bila shuruti.

Naahidi kuwa nitatii kanuni na sheria zote za shule na kufuata kikamilifu masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule au Walimu au yeyote mwenye mamlaka shuleni.

Naahidi pia kwamba nitajishughulisha na kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za Masomo, Uzalishaji Mali, Usafi na Michezo kwa muda wote nitakaokaa shule ya sekondari Lyamungo.

Nikishindwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zingine za shule, sheria ichukuliwe dhidi yangu.

Mimi (Jina la Mwanafunzi) ……………………………………………………………………….. sahihi

………………………..

Jina la Mzazi ………………………………………………………………… sahihi……………………………………

Jina la Mtendaji wa kijiji /Mtaa: …………………………………………………….……………………..

Sahihi …………………………………….. Mhuri ………………………………..

# KIAMBATANISHO C

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUMPA MKUU WA SHULE.**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya**…………………………………………………………..**

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi …………………………………………..

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:

A) Hali ya mwili :

- Mapigo ya moyo……………………………………………………………………..
- Haemoglobin…………………………………………………………………………
- Kundi la damu (Blood Group)……………………………………………………
- Mkojo ………………………………………………………………………………
- Kinyesi……………………………………………………………………………..
- Macho yana kasoro………………………………………………………………..
- Masikio yana kasoro……………………………………………………………
- Angalia: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa/Magonjwa.
  …………………………………………………………………………………….
  …………………………………………………………………………………….
  …………………………………………………………………………………….
  …………………………………………………………………………………….
  …………………………………………………………………………………….

B) *Amewahi/hajawahi/au /hana magonjwa yafuatayo:

a) Broanchial Asthem…………………………………………………………………..
b) Tuboreulosis………………………………………………………………………..
c) Epilese………………………………………………………………………………
d) Blood pressure……………………………………………………………………..
e) Peptic/D……………………………………………………………………………..
f) Sicklecells……………………………………………………………………………
g) Ukoma………………………………………………………………………………..
h) Venereal Disease (give type)………………………………………………….
i) Mental illness (ugonjwa wa akili)………………………………………………
j) Any other serious disease not mentioned above
   ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………

………………………………………

**SAINI NA MHURI WA DAKTARI/MGANGA**

**TAREHE …………………………………..**

- **Futa neno lisilohusika.**

## *KIAMBATANISHO D*

## FOMU YA MZAZI/MLEZI

(Ijazwe na Mzazi/Mlezi na mwanafunzi aje nayo shuleni.

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi): ……………………………………………………………………………………………………

wa mtoto (jina la mtoto) ……………………………………………………………………………………………………..

Ninakubali nafasi aliyotunukiwa mwanangu kwenda kusoma shule ya sekondari Lyamungo. Ninaahidi vilevile kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule ya sekondari Lyamungo katika kumlea kitabia, kimasomo, kikazi n.k. wakati wowote atakapokuwa shuleni Lyamungo Sekondari mpaka atakapomaliza masomo yake. Na kwa wakati wa likizo nitamtunza ipasavyo mpaka amalizapo likizo yake. Kadhalika ninathibitisha kuwa yote yaliyoelezwa na Mganga wa Mkoa/Wilaya ni sawa na zaidi ana tatizo/matatizo kama ifuatavyo:-

……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………

**…………………………………………………………….**
**SAINI YA MZAZI/MLEZI**
**TAREHE: …………………………………….**

Anwani yangu ya kudumu ni:

…………………………………………………………..

…………………………………………………………..

…………………………………………………………..

**Angalizo:** (Kila anuani hii inapobadilika tafadhali tujulishe)

Namba zangu za simu ni:

1. ……………………………………………..
2. ……………………………………………..
3. ……………………………………………..
4. ……………………………………………..

*Futa neno lisilohusika*

**KIAMBATANISHO E**

**SHULE YA SEKONDARI LYAMUNGO**
**S. L. P 3020**
**MOSHI**
**MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi : ……………………………………………………………………………………………………….
   Mwaka aliozaliwa: ……………………………………………………………………………………………………….
   Mahali alipozaliwa: ……………………………………………………………………………………………………..

2. Jina la Baba/Mlezi : ………………………………………………………………………………………………………
   Kazi ya Baba/Mlezi : ……………………………………………………………………………………………………….
   Mahali wanapoishi: ………………………………………………………………………………………………………
   Kijiji: ……………………………………………………………………………………………………
   Tarafa: …………………………………………………………………………………………………
   Wilaya: ………………………………………………………………………………………………..
   Anwani ya Baba/Mlezi:
   Ndugu:
   ……………………………………………………………………………………………………….
   ……………………………………………………………………………………………………….
   ……………………………………………………………………………………………………….

3. Majina ya ndugu wengine wanaohusika katika malezi ya mwanafunzi huyo.
   i. Ndugu: …………………………………………………………………………………………………………….
      Anwani yake: ………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….
   ii. Ndugu: …………………………………………………………………………………………………………….
      Anwani yake: ………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….
   iii. Ndugu: …………………………………………………………………………………………………………….
      Anwani yake: ………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….
      ……………………………………………………………………………………………………….

4. Maelezo mengine yoyote yatakayoweza kusaidia Uongozi wa shule katika kumlea mwanafunzi huyu.
   ………………………………………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………………………………………..
   Tafadhali fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni kwa Mkuu wa shule.

**Viambatisho na Fomu Muhimu.**

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jina.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**